

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TISA

KIKAO CHA PILI

02 NOVEMBA, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TISA

KIKAO CHA PILI – TAREHE 02 NOVEMBA, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2022 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2022*].

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2022 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2022*].

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi

Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**21. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI
CHAUREMBO (MBAGALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, nini kauli ya Serikali juu ya mapunjo ya fidia kwa Wananchi walioathirika na mlipuko wa mabomu Mbagala.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

22. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Mamlaka ya Mji Mdogo Shirati katika Wilaya ya Rorya itaanza kufanya kazi kama Mamlaka kamili.

23. MHESHIMIWA DOROTHY GEORGE KILAVE (TEMEKE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itamaliza mgogoro wa ardhi kati ya Wananchi na Serikali katika Kata ya Yombo Vituka.

WIZARA YA NISHATI:

**24. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE
(KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Wananchi wa Kitongoji cha Cheketu Somanga Kusini watalipwa fidia kupisha ujenzi wa miundombinu ya umeme.

**25. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE
(NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, nini mkakati wa Serikali kumaliza kero ya kukatikakatika kwa umeme Mikoa ya Kusini hasa Wilaya ya Masasi na Vijiji vyake.

WIZARA YA AFYA:

**26. MHESHIMIWA ABDUL-HAFAR IDRISSA
JUMA (MTONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupambana na visababishi vya maradhi yasiyoambukiza.

WIZARA YA KILIMO:

**27. MHESHIMIWA JUSTINE LAZARO NYAMOGA
(KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Bwawa la maji katika Kata ya Nyanzwa kwa ajili ya skimu ya umwagiliaji.

**28. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI
(TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha matokeo ya tafiti za kilimo yanawafikia Wakulima.

WIZARA YA MADINI:

**29. MHESHIMIWA YAHYA ALLY MHATA
(NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali ina taarifa juu ya upatikanaji wa madini Nanyumbu na Je, Wananchi wananufaikaje.

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

30. MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI (MALINYI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, Serikali haioni haja ya kutoa kipaumbele cha ajira kwa Majeshi yote nchini kwa Vijana waliohitimu JKT.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

31. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Mkalama.

32. MHESHIMIWA SAADA MANSOUR HUSSEIN (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kunusuru maisha ya Vijana wa kike kwa kudhibiti wimbi la mauaji Visiwani Zanzibar.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

33. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali haioni haja ya kupunguza eneo la Hifadhi ya Msitu wa Mbiwe ili litumike kwa matumizi ya Wananchi na shughuli za kiuchumi.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

34. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia Watoto wa mitaani ambapo kwa siku za karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

35. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Benki Kuu itaweka utaratibu kwa Serikali na Taasisi zake kuweka fedha Benki za biashara ili kuwa na mzunguko mzuri wa fedha.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

36. MHESHIMIWA AHMED ALLY SALIM (SOLWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Mwanangwa Mwakitolyo hadi Bulige Wilayani Kahama.

37. MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Bandari Kavu katika Mkoa wa Kigoma.

WIZARA YA MAJI:

38. MHESHIMIWA KATANI AHMED KATANI (TANDAHIMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini mradi wa maji wa Mkwiti utakamilika ili kupunguza tatizo la maji katika Kata ya Mangombya, Mkwiti na Litehu.

WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

39. MHESHIMIWA KAVEJURU ELIADORY FELIX (BUHIGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, kuna mpango gani kuweka Mazingira bora ya uwekezaji kilimo cha Michikichi pamoja na kiwanda cha kuchakata mafuta - Kigoma.

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima
na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2022 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2022*].

V. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):**

Kwamba , Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):**

Kwamba , Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu

wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC):

Kwamba , Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

**DODOMA
02 NOVEMBA, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**